# UPONYAJI

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha MPONYAJI. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MPONYAJI

1.Mponyaji?……………………………………………………

2. Kazi ya mponyaji…………………………………

3. Karama ya Uponyaji…………………………………………

4. Wokovu………………………………………………………

5. Maombi……………………………………………………….

6. Yesu ni Mponyaji…………………………………………

9.Kuokoka………………………………………………………

10. Mwisho……………………………………………………

# 1. MPONYAJI ?

Mponyaji ni mtumishi wa Yesu mwenye huduma ya uponyaji ya kanisa la waliokoka.Yesu humtumia kuponya wagonjwa hata yale yasiyowezekana kwa matabibu na wanadamu.Mfano wa magonjwa aliyoponya Yesu ni homa,safura, kupooza na ugonjwa wa kutoka damu na ukoma.

**Luka 14:2– 4**

" Na tazama, mbele yake palikuwa na mtu mwenye **ugonjwa wa safura.** Wao wakanyamaza. Akamshika, akamponya, akamruhusu aende zake. "

**Mathayo 4:23 –24**

"Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya **ugonjwa** na udhaifu wa kila namna katika watu.

Na habari zake zikaenea katika Shamu yote; wakamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na maradhi mbalimbali na mateso, wenye pepo, na **wenye kifafa,** na wenye **kupooza;** akawaponya. "

**Marko 6: 5**

"Wala hakuweza kufanya mwujiza wo wote huko, isipokuwa **aliweka mikono yake juu** ya **wagonjwa** wachache, akawaponya. "

Yesu aliponya watu kwa kuwakea mikono au kutamka neno la uponya. Kuwakea mkono mgonjwa ni njia nzuru ikiwa mgonjwa upo naye ana kwa ana na ile ya kutamka neno mgonjwa kama yu mbali yaani hayupo karibu nawe. Zipo aina zingine za uponyaji kama kutumia nguo kama leso,mafuta na kivuli cha mtumishi wa mungu. Yesu akikupa huduma ya uponyaji ifahamu karama yako ya uponyaji ni ya aina gani? Na umfuate Yesu ktk kutumika ndipo utafanikiwa usisahau msamaha ni muhimu ktk uponyaji nawe una Roho mt

## 2.KAZI YA MPONYAJI

Kazi ya mponyaji ndani ya kanisa la waliokoka wenye huduma ya kuponya wagonjwa ni kama zifuatazo:

1) Kuponya wagonjwa ambao hajafika cheo cha baraka ya afya ya Yesu
2) Kuponya wagonjwa wachanga kiroho ambao hawafikia ufahamu wa cheo cha kristo yaani.
3) Kuponya wagonjwa waliosamehewa dhambi kwa kuokoka lakini wanadumu ktk maombi ya kuponywa magonjwa yao na watembea ktk Imani au wana Imani au shauku ya kuponywa`ila bado hawajaponywa siku walipokoka kama ilivyo kawaida ya haki ya msamaha nduguye ni uponyaji. **(Zab 103:3)**
4) Kuponywa wagonjwa waliokoka wezi wa fungu la kumi au wanaoiba zaka na kutotii magizo ya mungu kupita manabii mfanohoma Ukaufu na Kifua Kikuu,.**(kumb. 28)**
5) Kumponywa wagonjwa wenye magonjwa yaliyoshindikana kwa matabibu na wanadamu waliokoka mfano; viwete,vipofu,bubu na viziwi.
6) Kuponya wagonjwa kwa njia mikutano/maombezi ya uponyaji kwa waliokoka

Kazi ya mponyaji nje ya kanisa la waliokoka wenye huduma ya kuponya wagonjwa ni kama zifuatazo:

1) Kuponya wagonjwa ambao hawajaokoka mmoja mmoja au kwa njia mikutano/maombezi ya uponyaji kwa wasiokoka, wenye dhambi au wasioamini
2) Kuita watu waliotayari kuokoka mwisho mkutano au maombezi ya uponyaji Yesu alisema mavuno ni mengi ...;hivyo ni kazi ya kanisa (waombaji) kuomba mitume,wahubiri,nabii,wainjilisti wakubwa moja ya kazi yao ni kuhubiri ambao ni wachache ..

# 3.KARAMA YA UPONYAJI

Karama ya uponyaji wa magonjwa Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka nataka ufahamu huu juu ya uponyaji zipo za aina mbalimbali au kadhaa ninazozifahamu kibiblia na nilizozishudia kwa macho waliokoka na kujazwa roho mtakatifu na kupewa roho mtakatifu karama hiyo ambayo ukiicochea sana inazaa huduma ya uponyaji ni:

1) Kuwekea mikono juu ya wagonjwa na kupata afya

**Marko 16:15-18**

" watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; **wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.** "

2)Yesu kusema nawe neno la Uponyaji

**Zaburi 107: 19—20** "Wakamlilia Bwana katika dhiki zao, Akawaponya na shida zao. Hulituma **neno lake, huwaponya**, Huwatoa katika maangamizo yao. "

3)Kupaka wagonjwa mafuta ya mzeituni yaliyoombewa.

**Marko 6.13** "Wakatoa pepo wengi, **wakapaka mafuta** watu wengi waliokuwa **wagonjwa,** wakawapoza. "

4)Roho mtakatifu kusema nawe kwa ishara Mfano kusihisi tumbo linaumwa kisha kuletewa,kukutana au kupewa taarifa saa ile ile ya mtu tumbo linaumuuma pengine amelazwa anakuomba umuombee na ghafla ukimuombea maumivu ya tumbo madogo unakuta yameisha na ukitaka taarifa kwa mgonjwa uliyemuombea hata saa ile unakuta naye ameponywa.

5)kivuli chako ukipita kikiangukia mgonjwa anaponywa.

6)Nguo zinazotoka ktk mwili wako mfano shati,suruali sketi,leso na kuwekea mgonjwa naye anaponywa

7)Kuombea nguo mfano leso kupelekwa kwa mgonjwa aliye nyumbani au hospitalini na kuwekea juu ya mgonjwa naye anaponywa

# 4. YESU YA MPONYAJI

Yesu ni Mponyaji mkuu yeye ndiye Bwana atumaye neno lake kumponya amtaye. Mfano na kielelezo kwa watumishi wa Mungu wenye huduma ya uponyaji. Kuweka msingi ktk huduma yako ya uponyaji au karama mfuate Kwa kutenda yale aliyosema kuhusu uponyaji au kutafuta wagonjwa au watu waliowaponya yeye na walioandikwa ktk biblia na kuwahudumia hasa ile mistari biblia ya vitabu vya injili yenye neno kuponya; Wagonjwa hao wapo wa homa, safura, kupooza, ugonjwa wa kutoka damu ,viwete,vilema,bubu , vipofu,pepo + kifafa, pepo +kipofu+bubu,.

**Mathayo : 4:24** "Na habari zake zikaenea katika Shamu yote; wakamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na maradhi mbalimbali na mateso, **wenye pepo,** na wenye **kifafa,** na wenye **kupooza; akawaponya**. "

**Mathayo 9:20 – 22** " Na tazama, mwanamke aliyekuwa na **ugonjwa wa kutoka damu** muda wa miaka kumi na miwili, alikuja kwa nyuma, akaugusa upindo wa vazi lake. Kwa maana alisema moyoni mwake, Nikigusa tu upindo wa vazi lake nitapona. Yesu akageuka, akamwona, akamwambia, Jipe moyo mkuu, binti yangu; imani yako imekuponya. Yule mwanamke akapona tangu saa ile. "

**Mathayo 12.22** "Wakati ule akaletewa mtu mwenye **pepo, kipofu,** naye ni **bubu; akamponya**, hata yule bubu akanena na kuona. "

**Mathayo 15:30** " Wakamwendea makutano mengi wakimletea **viwete, vipofu, mabubu**, **vilema,** na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake; **akawaponya;** "

**Luka 14:2 – 3** "Na tazama, mbele yake palikuwa na mtu mwenye **ugonjwa wa safura**. Yesu akajibu, akawaambia wana-sheria na Mafarisayo, Je! Ni halali kuponya siku ya sabato, ama sivyo? " Wao wakanyamaza. Akamshika, **akamponya,** akamruhusu aende zake.

# 4.WOKOVU WA MPONYAJI

**Wokovu** ni maisha ya mtu aliyeokoka kama matokeo ya kutendewa mema na mungu mfano miujiza,uponyaji,kutolewa pepo au kufunguliwa,kubarikiwa,kutajirishwa,kupewa ulinzi wa malaika , kujazwa furaha,Amani,Haki and Upendo.

Wokovu kwa waliokoka uletwa kwao na kudhihirika ktk maisha ya kila siku kutokana yupo chini ya huduma ipi ya kanisa pia na huduma iliyo ndani yako au karama unapochochea au kuitumia kupenda kanisa kama Yesu alivyoamuru yaani kuitumia kuhudumia wenzako waliokoka.

Wokovu wa mponyaji ni maisha mapya anayotakiwa kuishi mtumishi wa Yesu mwenye huduma ya uponyaji ili kutunza huduma yake na Karama ya uponyaji. Yafuatayo ni baadhi ya mambo ya kuzingatia :

1) Kumcha Mungu yaani kuchukia uovu kiburi, majivuno na njia mbovu
2) Kuombea wagonjwa waliokoka au wasiokoka waliopewa neema kwa kuongozwa Roho mtakatifu
3) Kuombea wagonjwa waliokoka wafike kanisani siku ya sabato au siku saba ya kukusanyika watakatifu ,wakristo au waliokoka kwa ajili ya Bwana Yesu mfano Jumapili na kuponywa magonjwa yao.
4) Roho Mtakatifu akuongoze ktk kweli ufikie utukufu wa kushudiwa na watu una dhambi na roho mtakatifu ndani yako maisha yako ya wokovu huna dhambi mbele za mungu na yesu amekuweka huru kutoka ktk utumwa na dhambi umekuwa mwana wa Mungu kama unakaa nyumbani maana yake hutendi dhambi
5) Uwe mwenye huruma na msamaha wa wenye dhambi waliopooza.

.

# 5. MAOMBI

;” Maombi ya Mponyaji au mtumishi wa Yesu au mtumishi wa mungu  ktk utumishi wake au ndio umeokoka na umefahamu umepewa na roo mtakatifu karama ya uponyaji:=>

1) Kuomba mungu akukutanishe na wagonjwa waliokoka ambao hawajatendewa haki naye kupitia neema yake ya karama na huduma ya uponyaji iliyo ndani yako  kama mtumishi wake au mtu uliyeokoka anaweza kukutumia kuwaponya kufumba na kufumbua.
2) Kuomba mungu akukutanishe na wagonjwa wasiokoka ambao ni wenye dhambi  kupitia neema yake ya karama na huduma ya uponyaji iliyo ndani yako  kama mtumishi wake au mtu uliyeokoka anaweza kukutumia kuwaponya kufumba na kufumbua. Na jina la Yesu linatukuzwa.
3) Kuwaombea wale waponywao na mungu wenye dhambi wakutane naYesu na kubadilishwa maisha yao ya dhambi kwa kuokoka kupitia uponyaji wa ugonjwa au magonjwa.
4) Kuwaombea wale waponywao na mungu waliokoka wakutane kupitia uponyaji wa ugonjwa au magonjwa yao na ikiwa walikuwa na tabia fulani ya dhambi au uovu  wabadilishwe na Yesu kupitia huo uponyaji na kuacha au kuuacha  ambao pengine ulisabisha huo ugonjwa au magonjwa.
5) Kuomba mungu akukutanishe na wagonjwa wa kuwaponya walioandikwa ktk vitabu vya injili na mungu akutumie kuwaponya nao ni  wenye homa, safura, kupooza, ugonjwa wa kutoka damu ,viwete,vilema,bubu , vipofu,pepo + kifafa, pepo +kipofu+bubu,.
6) Maombi kumshukuru mungu kila ukutumiapo kuwaponya watu.

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**


Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 9332

**MWENGE— DAR-ES-SALAAM TANZANIA**



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034